

# KUENDELEZA LUGHA YAKO YA NYUMBANI

NEWCOMER  
PARENT  
RESOURCE  
SERIES

Utafiti unaonyesha kwamba kuendeleza lugha yako ya nyumbani haitamfaidi tu mtoto wako kwa kutangamana na kihisia, bali kunaweza pia kuboresha ujuzi wake wa utambuke, kuongezea utendakazi wa jumla wa ubongo, na kumsaidia kujifunza lugha mpya.

## Kuna sababu nyingine za kuendelea kutumia lugha yako ya nyumbani na mtoto wako.

- Familia yako itaongea kwa urahisi zaidi wao kwa wao na itaweza kuelezea hadithi ngumu na kushiriki vichekesho na nyimbo.
- Wewe na mtoto wako mtahisi mko karibu sana.
- Mtoto wako atasikia na kujifunza kutumia lugha ambayo ina ukwasi na dhahiri.
- Mtoto wako ana uwezo zaidi wa kushiriki hisia zake na wewe.
- Wewe na mtoto wako mnaweza kuelewana vizuri zaidi.
- Mtoto wako ana uwezo zaidi wa kukusikiliza.
- Mtoto wako anaweza kuhisi anastahili na ajivunie lugha na utamaduni wake.
- Mtoto wako anaweza kuongea na wanafamilia wengine na marafiki wa familia.
- Mtoto wako ana uwezo zaidi wa kuongea lugha zote kwa njia changamani zaidi. Hii inaweza kusababisha ufanisi zaidi shuleni.

Wakati watoto wageni wanapoanza kuhudhuria mpango wa huduma ya watoto au kwenda shule kwa mara ya kwanza, huenda wasielewe au kuongea Kiingereza chochote, lakini hiyo ni sawa! Katika miezi michache, watoto wengi hujifunza Kiingereza kiasi. Na mtoto wako anavyoendelea kukomaa, atakuwa na uwezekano zaidi wa kuongeza Kiingereza zaidi na zaidi.



## Mapendekezo ya Kuendeleza Lugha Yako ya Nyumbani:

- Daima tumia lugha yako ya nyumbani na mtoto wao na himiza wanafamilia wote kuitumia.
- Ikiwa mtoto wako anaongea Kiingereza, mwulize akuambie alichokisema kwa lugha yako ya nyumbani. (Mara ya kwanza unaweza kuisema kwa lugha yako ya nyumbani, ili waweze kujifunza.)
- Tumia michezo, nyimbo na hadithi kufanya lugha ivutie zaidi.
- Kuwa na mazungumzo ya kweli, badala ya kumwambia tu mtoto wako cha kufanya.
- Ikiwa mtoto wako anakataa kuongea lugha yake ya nyumbani, unaweza kuchagua nyumba au muda maalum (k.m. wakati wa chakula cha jioni) kuzungumza tu lugha yako ya nyumbani.

Tembelea [cmascanada.ca/cnc/parents](https://cmascanada.ca/cnc/parents) kwa maelezo zaidi ya lugha mbalimbali ya wazazi



SUPPORTING CHILD CARE IN THE SETTLEMENT COMMUNITY / SOUTIEN DE LA GARDE DES ENFANTS DANS LA COMMUNAUTÉ DE RÈGLEMENT

Funded by: Immigration, Refugees and Citizenship Canada / Financé par : Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada